



TANZANIA REVENUE AUTHORITY

**ISO 9001:2008 CERTIFIED
CHUO CHA KODI**

MAHAFALI YA KUMI

Chuo cha Kodi (ITA) kinawatangazia Wahitimu wa masomo wa mwaka 2016/2017 na wananchi wote kwa ujumla, kwamba **Mahafali ya Kumi** yatafanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Kodi siku ya Jumamosi tarehe **18 Novemba, 2017**.

Wahitimu watakaopenda kushiriki katika Mahafali wanatangaziwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kuthibitisha ushiriki kwa maandishi kabla ya tarehe **10 Novemba 2017** kwa Naibu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala.
2. Kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali watakaovaa majoho ni wahitimu wa Shahada ya Usimamizi wa Forodha na Kodi (BCTM), Astashahada ya Uzamili ya Uongozi wa Forodha ya Africa Mashariki (PGCCA) na Wahitimu wa Stashahada ya Uzamili katika Kodi (PGDT) . Hivyo wahusika wanatakiwa kulipia joho kiasi cha shilingi 50,000 tu na kuwasilisha stakabadhi ya malipo kwa Naibu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala kabla ya tarehe 10 Novemba 2017.
3. Malipo yote yafanyike kupitia Benki ya CRDB, Akaunti **ITA Fee Collection Account No. 0150303205600**.
4. Wahitimu waliothibitisha ushiriki na kulipia watatakiwa kuchukua majoho na kufanya mazoezi siku ya Alhamisi tarehe **16 Novemba 2017** katika Ukumbi wa Chuo cha Kodi kuanzia saa tatu asubuhi.

Wahitimu watakaoshiriki mahafali watapaswa kugharamia usafiri na malazi yao.

“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”

**Mkuu wa Chuo
Chuo cha Kodi
S. L. P. 9321, Dar es Salaam
E-mail: ita@tra.go.tz**